Jarida la Shirika la Uboreshaji Mifereji ya Asili na Uhifadhi wa Mazingira (TIP)

Maendeleo ya TIP

Toleo la 8 Novemba 2005

Tunza kumbukumbu zako sawia

Utunzaji wa kumbukumbu ni taratibu za kuhifadhi taarifa zozote ziwe za mtu binafsi au kikundi kwa ajili ya matumizi ya baadae. Utunzaji sahihi wa kumbukumbu ni muhimu sana katika kikundi chako. Kumbukumbu zinaweza kuwekwa katika makundi matatu: taarifa za shughuli za kikundi, taarifa za mapato na matumizi ya fedha na dondoo za mikutano.

Faida za kutunza kumbukumbu vizuri

1. Inasaidia wanakikundi kukumbuka matukio.
2. Inataarifu wanakikundi nini kinachoendelea na kupunguza kutoaminiana.
3. Hupima maendeleo hivyo kuweza kuelewa ni wapi penye mapungufu na palipoimarika.
4. Hufuatilia shughuli za kikundi na kuweza kutoa maamuzi.
5. Huboresha uwazi na uwajibikaji.
6. Inakidhi taratibu za kisheria.

Wanakikundi hawana budi kuelewa kumbukumbu zote zilizohifadhiwa na pia zifafanuliwe kwa wale wasio na uwezo wa kusoma. Kumbukumbu hizi hutunzwa na mjumbe/wajumbe walioteuliwa na wanakikundi kwa madhumuni ya maendeleo ya kikundi ili kufikia malengo waliyojiwekea. Wanakikundi wanastahili kupata na kutumia kumbukumbu za kikundi kulingana na katiba yao inavyosema.

Utaratibu wa utunzaji wa kumbukumbu ufanyike kila mara na endapo kutatokea tukio muhimu. Takwimu na taarifa zote za kikundi huhifadhiwa kikamilifu katika vitabu maalumu vya kumbukumbu na sio kwenye karatasi. Uangalifu wa hali ya juu unatakiwa wakati wa kuhifandi kumbukumbu muhimu kama mikataba, taarifa za maombi, shughuli zilizopagwa kwa kipindi fulani na taarifa za fedha (mapato na matumizi).

Maswali ya kujiuliza kwa utunzaji mzuri kumbukumbu

1. Ni taarifa gani zinazotakiwa kuhifadhiwa?
2. Jinsi ya kuhifadhi taarifa?
3. Ni muda gani taarifa inatakiwa kuhifadhiwa?
4. Nani mwenye haki ya kutumia taarifa zilizohifadhiwa na kwa wakati gani?
5. Ni taratibu zipi zitumike kufuta kumbukumbu za muda mrefu?

Tuzo ya Nane Nane

Shirika la TIP lilishiriki maonyesho ya 13 ya Kilimo na Mifugo (Nane Nane) 2005, yaliyoandaliwa na TASO kanda ya kaskazini katika viwanja vya Themi, Arusha. Ujumbe wa TASO mwaka 2005 ni " Kilimo bora ni nyenzo muhimu ya kuondoa aina zote za umaskini".

Wageni wakipanda Mlima Matumaini katika banda la TIP.

Banda la TIP lilikuwa na sehemu zilizoonyesha kitalu cha miti, kilimo mchanganyiko, mbinu mbalimbali za uvunaji maji, matuta, majiko sanifu, hifadhi ya nafaka na masoko. "TIP imeonyesha vitu ambavyo vinaweza kumtoa mkulima kwenye umaskini" alisema Mgeni rasmi, Mhe. Abdulrahman Kinana, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. TIP ilipata ushindi wa kwanza katika kundi la mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojishungulisha na kilimo na nafasi ya tatu katika ushindi wa jumla wa maonyesho. Shirika linatoa shukrani kwa wote waliohusika kwa kujituma kwao na kuliwezesha shirika kupata mafanikio mazuri katika maonyesho.

Jinsi ya kumtambua kiongozi bora

Kiongozi ni mtu yeyote aliyechaguliwa aongoze waliomchagua ili kufikia malengo waliyojiwekea. Baadhi ya viongozi ni wa kiimla. Viongozi hawa hurithi madaraka kutoka kwa ndugu zao waliowatangulia. Katika hali hii uchaguzi wa kidemokrasia huwekwa pembeni na wakati huo watu wengine wenye vipaji vya uongozi wanaachwa bila kupewa fursa ya kuonyesha uwezo wao wa uongozi.

Kwa kutumia majadiliano ndani ya kikundi, kuhusu sifa na kumchagua mwanakikundi mwenye sifa za uongozi, wanakikundi hupata ufahamu/ujuzi wa kuongoza kikundi au kubeba majukumu fulani ndani ya kikundi.

Ujuzi katika uongozi ni muhimu kwani huwafanya wanakikundi kuwa na furaha, mwelekeo na ufanisi, hatimaye kikundi hufikia malengo yake. Kukiwa na uongozi bora, wanakikundi huelewa nini kinatarajiwa kutoka kwao hali ambayo huwatia moyo wa kufanya kazi kwa pamoja.

Hebu tutazame sifa za uongozi.

Kitu kinachohitajika kwa kiongozi ni kupata ujasiri kutokana na watu anaofanya nao kazi tofauti na hivyo hakuna atakayemfuata.

Inaendelea ukurasa wa 2.

Sifa za kiongozi bora

- Mchapakazi, anayehamasisha wenzake
- Mwenye bidii, anayejituma, Muadilifu
- Anajiheshimu, Anayetegemewa
- Sio mlevi
- Asiye na aibu
- Mwerevu
- Mwaminifu
- Mvumilivu
- Mwepesi kuwasiliana
- Anapenda ushirikano
- Anapenda mabadiliko

Sifa za kiongozi mbovu

- Hana uwezo wa kuongoza wengine
- Si mvumilivu
- Hutawala kiimla
- Asiyetegemewa
- Hapendi ushirikiano
- Mwenye upendeleo
- Mbinafsi
- Ana hasira na mkatili

Lishe ya Muhogo

Chakula hiki kina kiasi kidogo cha mafuta, kolestro na sodiamu. Pia ni chanzo kizuri cha Manganizi na Vitamini C.

Wanga 97% - Mafuta 1% - 2% Protini

Jinsi ya kumtambua kiongozi bora

Inatoka ukurasa wa 1.

Wanaoongozwa wanatakiwa kuhakikishiwa kuwa kiongozi wao ni muadilifu, mwaminifu na ana mamlaka.

Kuna aina tatu za mamlaka:

1. Cheo. Hii hujumuisha wadhifa au nafasi aliyopewa mtu, mfano Mwenyekiti n.k.
2. Utu. Baadhi ya watu wana mamlaka kulingana na tabia au sifa zao kiasili
3. Taaluma. Mamlaka ya namna hii yanatambulika kutokana na taaluma ya mtu au kuwa na uzoefu wa eneo husika.

Nyakati zilizopita , kulikuwa na utaratibu wa kuwatambua viongozi kulingana na nafasi zao katika jamii. Kwa mfano, baadhi ya jamii za Kiafrika, uongozi ulikuwa wa kiukoo au wa kurithisha kizazi kimoja hadi kingine. Hata kama watu hawa hawakuwa na sifa za kuwa viongozi imara. Kwa sasa, viongozi huchaguliwa kulingana na utu na uwezo wao kitaaluma. Baadhi ya miradi ya jamii inayopata msaada kutoka TIP, hupata mafunzo ya kuimarisha vikundi. Wakati wa mafunzo ya jinsia na uongozi, wanakikundi hujifunza majukumu ya mwanamke na mwanaume katika kikundi na miundo ya uongozi inayoweza kuleta ufanisi wa kikundi.

Hebu tutazame tabia za kiongozi.

Kiongozi anatakiwa kuwa na ujasiri na uadilifu. Ujasiri ni uwezo wa kutenda kile kinachotakiwa bila kujali gharama au hasara. Uadilifu ni uwezo wa kutekeleza majukumu kihalali bila kujali kuwa kuna vishawishi au wasiwasi kutoka kwa watu. Hizi ni sifa muhimu zinazaotakiwa ili kupima uwezo wa mtu.

Viongozi wanatakiwa wapende kushirikiana na wenzake, wawe na shauku na kujua jinsi ya kuwashirikisha watu wengine ujuzi alionao. Kiongozi anatakiwa awe ni mtu mwenye kukubali mabadiliko kwa masuala ambayo hana uzoefu nayo.

Kiongozi wa kweli ni yule anayependa kujifunza kila wakati na anayeweza kuchukuliana na hali zozoote. Watu watamfuata kiongozi wao bila kujua wamechukua nafasi ya wanaoongozwa. Matokeo yake kiongozi hufanya kila mwanakikundi kufanya kazi kulingana na mtazamo waliojiwekea kwa mafanikio ya wote.

Muongozo wa nafasi za uongozi katika kikundi

Mwenyekiti

- Kuitisha mikutano na vikao vya majadiliano.
- Kuongoza mikutano.
- Kutia moyo wajumbe kushiriki katika majadiliano, kufanya maamuzi na kushiriki katika kazi.
- Kuhakikisha matumizi sahihi ya katiba ya kikundi.
- Kuhakikisha katibu na mhazini wanawajibika kulingana na wajibu wao.
- Kuhakikisha malipo ya michango ya wanachama.
- Kugawa kazi na majukumu.
- Kuhakisha kuwepo kwa amani na utulivu katika kikundi.
- Kuwakilisha kikundi katika mikutano na taasisi nyengine.

Katibu

- Kuandaa agenda na dondoo za vikao na mikutano.
- Kutunza kumbukumbu zote ikiwa pamoja na mahudhurio ya mikutano na kazi za kikundi.
- Kusoma dondoo za mikutano.
- Kupokea na kutunza mawasiliano yoyote ya kikundi na kutoa taarifa kwa kikundi.
- Kutunza vitabu vya kumbukumbu.
- Kumsaidia mwenyekiti.

Mhazini

- Kutunza taarifa za fedha za kikundi.
- Kulinda na kuratibu michango ya wanakikundi.
- Kutoa risiti kwa kila pesa inayopokelewa na kulipwa.
- Kutunza vitabu vya mauzo na manunuzi na vya kupokelea pesa.
- Kumsaidia mwenyekiti.
- Kutoa taarifa za mapato, matumizi, salio na statimenti ya benki kwa wanakikundi.

Wajumbe wa kamati

- Kuandaa ajenda na tarehe za mikutano.
- Kuwasilisha kazi za kamati.
- Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wanakikundi.
- Kushiriki katika utoaji wa maamuzi.
- Kutekeleza mipango baada ya kufanyiwa maamuzi.
- Kusimamia matumizi sahihi ya katiba ya kikundi na kutoa adhabu kwa mwanakikundi atakayekwenda kunyume.
- Kugawa kazi na kuhamasisha ushiriki.
- Kuwasiliana na watoa mada muhimu, vikundi na taasisi mbali mbali.
- Kuhifadhi mambo nyeti katika kikundi.
- Kuandaa semina na mafunzo.
- Kuwakilisha kikundi.

Saladi ya muhogo

Mahitaji

- Mihogo iliyokatwakatwa vipande vya ½ inchi katika umbo mraba vikombe 6
- Chumvi kijiko 1 cha chai
- Mayonaizi ½ kikombe
- Vinega 1/8 kikombe
- Vitunguu saumu 2 vilivyotwangwa
- Coriender fungu moja liliokatwakatwa
- Pilipili manga
- Vitunguu maji 2 vilivyokatwakatwa
- Pilipili hoho 1

Maandalizi

Menya muhogo, pasua katikati na uondoe mzizi. Katakata vipande vya ½ inchi vyenye umbo mraba. Chemsha maji katika sufuria ya wastani. Weka chumvi na mihogo na chemsha kwa muda wa dakika 30. Usichemshe sana, epua na chuja maji.

Changanya mayonaizi, vinega, vitunguu saumu, pilipili manga na cilanto katika chombo kingine.

Changanya mchanganyiko wa mayonaizi na mihogo. Tikisa. Weka kwenye vitunguu na pipipili hoho. Hifadhi kwenye jokofu.

WATU

Wanafunzi wafanya kazi TIP

Rose Missana na Ritha Swai ni wanafunzi wa mwaka wa pili kutoka Chuo Cha Maendeleo ya Jamii (CDTI), Rugemba Iringa. Walijiunga TIP kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo kutoka tarehe 18 Julai – 19 Septemba 2005. Wamelisadia shirika kukusanya takwimu za awali za mradi wa umwagiliji wa Nganjoni unaotekelezwa na TIP wilaya ya Moshi vijijini. Wameshiriki katika mafunzo ya usajili wa Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) za wakulima wa wilaya ya Arumeru.

Tanzia

Bw. Josepoh Mkwama alikuwa Afisa Mshauri wa TIP katika progamu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMSDP), alifariki dunia tarehe 16 Agusti 2005. Katika kipindi cha utumishi wake ndani ya TIP, Joseph alikuwa muadilifu, aliyejituma na aliyependa kushirikiana sana na wenzake. Joseph atakumbukwa daima na wafanyakazi wenzake. Shirika linatoa salamu za rambirambi kwa mkewe, watoto na ndugu zake. Mungu ailaze roho ya marehemu Joseph mahali pema peponi. Amina.

Joseph akifanya kazi idara ya habari ya TIP kwenye maonyesho ya Nane Nane 2005.

Habari za Wilayani

Arumeru

Kilimo hai kwa hifadhi ya ardhi endelevu

Soko huria limesababisha madhara makubwa kwa wazalishaji wadogo. Wazalishaji wadogo wa mbogamboga wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na soko huria kutokana na kushindwa kumudu ongezeko la bei za mbolea na viuatilifu. Viuatilifu na mbolea za viwandani zina gharama kubwa.

Mradi mdogo wa kilimo hai ulianza na wakulima 10 wa kijiji cha Ilkisongo. Mradi ulipata mafanikio baada ya majaribio kadhaa kufanyika. Baadhi ya wakulima walio katika maeneo ya TIP walionyesha kuvutiwa na mafanikio ya mradi baada ya kutembelea Ilkisongo. Wakulima 8 kutoka Nduruma na 10 kutoka Ambureni wanatumia kilimo hai kuzalisha mazao. Mazao yanayozalishwa kutokanayo na kilimo hai hupata bei nzuri katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Kilimo hai kina faida nyingi. Baadhi ya faida zimeainishwa kama ifuatavyo:

- Dawa/viuatilifu vya asili vinavyotumika katika kilimo hai havina athari ya kiafya kwa binadamu wala wanyama.
- Dawa/viuatilifu vya asili vinavyotumika hupatikana kwa bei na fuu au bure.
- Ni rahisi kutumia njia hii ya kilimo kulinganisha na nyengine.
- Huongeza rutuba ya ardhi.

Lushoto

Matunda ya pears yapata bei nzuri

TIP iliendaa mafunzo ya Mwangaza wa Biashara kwa wakulima wa kata ya Sunga (Tema complex) mwaka 2003. Mafunzo yaliwawezesha wakulima kuwa na mtizamo wa kibiashara katika miradi wa kilimo. Wamekuwa na uwezo wa kulikabili soko moja kwa moja na kutotumia madalali na kufanikiwa kupata kipato kikubwa. Kabla ya hapo debe 3 (Kg 50) za pears ziliuzwa kwa Sh 150/=, wakati hivi sasa debe moja huuza kwa sh. 400/=. Wakulima wa jirani na vijiji vya jirani wameamua kuiga mtindo huu wa biashara ili nao wapate mafanikio kama wenzao wa Sunga.

Katibu Tawala wa Mkoa Kilimanjaro Bi. N. M. Sumari, akipata maelezo kutoka kwa wanakikundi wa Bere - Chome, alipotembelea wilaya ya Same tarehe 26 Septemba 2005.

Mwanga

Wakulima wahamasika baada ya ziara ya mafunzo

Wakulima 15 kutoka katika maeneo ya TIP Wilayani Mwanga, walifanya ziara ya mafunzo Mamba Myamba wilayani Same mwezi Septemba 2005. Walivutiwa na jinsi kilimo cha tangawizi kinavyoweza kubadilisha kipato chao. Wameagiza kilo 500 za mbegu ya tangawizi baada ya kutoka ziara ya mafuzo. Wakulima wamegundua kuwa kilimo huenda kikibadilika si kuwa kulima kitu walichozoea. Wameamua kubadilisha mazao yao na kuanza kuotesha tangawizi ambayo hukua vizuri katika maeneo ya Ngwale, Chunguli, Kwa Mlombola, Makungu na Msangai.

Mpango shirikishi wa ardhi kupunguza migogoro

Kwa muda wa miaka zaidi ya mitatu, Kijiji cha kileo, Mwanga kimekuwa katika mgogoro na wafugaji wa kijiji cha jirani cha Makuyuni, Moshi vijijini. Mifugo kutoka Makuyuni imekuwa ikilishwa katika kijiji cha Kileo na wakati mwingine kuharibu mazao yaliyo shambani. Pamoja na hayo kijiji cha kileo hakikuwa na mpango wa matumizi bora wa ardhi ambao ungetenga maeneo ya malisho ya mifugo, makazi na kilimo.TIP inawezesha mpango wa matumizi bora wa ardhi katika kijiji cha Kileo. Mipango itakayopitishwa itasaidia kuondoa migogoro ya mipaka kwa njia za kisheria na kuweka mikakati ya kutatua kwa mfano, migogoro inayohusu mifugo na matumizi mengine ya ardhi ndani ya kijiji.

Same

Upandandaji wa miti waongeza mavuno

TIP ilianza kufanya shughuli kwa kushirikiana na wakulima wa kikundi cha watumia maji cha Bere mwaka 1990. Upandaji wa miti ulikuwa moja ya shughuli zilizolengwa. Miti zaidi ya 300,000 ilioteshwa. Asilimia 60 ya miti iliyooteshwa imefanikiwa kukua vizuri yaani miti 180,000. “Faida ninazopata ni nyingi katika shamba langu kwa kupanda miti. Hunipatia kivuli, kuni, mbao, fito, dawa, hupunguza mmomonyoko wa udongo na kuongeza mbolea”. Alisema Mzee Omberi, mwanachama wa kikundi. Hali ya mazingira ya Bere imeboreka, miti iliyooteshwa imesaidia kupunguza mmomonyoko wa udongo na kuongeza uzalishaji.

Viazi mviringo vyaboresha maisha

Kabla miaka ya 1990, mazao ya biahara katika eneo bonde la mamba yalikua kahawa na miwa. Hivi leo zao kuu la biashara na chakula ni viazi mviringo. Baada ya kupata mafunzo ya utunzaji wa ardhi kutoka TIP, wakulima wameweza kuboresha ardhi yao kwa kutengeneza matuta. Mzee Zakayo Mgwena anasema, “Hali ya udongo wa Mamba Mweteni, hufanya viazi kuwa na ubora wa hali ya juu kulinganisha na vinavyotoka katika maeneo mengine ya Tanzania” Viazi huvunwa baada ya meizi mitatu hadi minne na kutoa mwanya wa kuotesha mazao mengine. Mzee Zakayo alisema kuwa, zao hili limewezesha upatikanaji wa chakula na kuongeza kipato kinachowawezesha kulipia ada za shule na kujenga nyumba bora.

TIP ni shirika lisilo la kiserikali la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji wa Mifereji Asili na Mazingira lililosajiliwa tangu mwaka 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lililoundwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama Mpango wa Uboreshaji Mifereji ya Asili chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV).

TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya umwagiliaji kwa mifereji ya asili.

Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili, kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo ya vyanzo vya maji nchini Tanzania.

TIP inalenga kuhudumia vikundi vidogo vya wakulima (me na ke) vilivyo katika maeneo yenye umwagiliaji Tanzania.

Kifurushai cha TIP

1. Uimarishaji wa vikundi na Jinsia
2. Ushirikishwa wa Matumizi bora ya ardhi
3. Uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji
4. Kuyakabili masoko na uendelezaji wa miradi ya kilimo

SHUKRANI

Shirika la TIP linapenda kutoa shukrani za pekee kwa:

NOVIB, UBALOZI WA JAPANI, UBALOZI WA UHOLANZI na SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP) Kwa ufadhili wa shughuli za TIP

Tuandikie

Tuma maoni yako, mapendekezo, ushauri, hadithi na mawazo yako kwa kutumia anwani ya TIP, andika jina lako kamili na anwani yako

TIP
S.L.P. Box 8909, Moshi - Kilimanjaro
Simu : 027 53025 / 54232
Faksi: 027 51124

Barua pepe: tip@tiptz.org
Mtandao: www.tiptz.org

Pata hati ya matumizi ya maji

Serikali ya Tanzania inaratibu vyanzo vya maji kwa kuvigawa katika maeneo nane yajulikanayo kama maeneo bonde ya mito. Eneo Bonde la Mto Pangani ni mojawapo ya maeneo haya. Eneo hili lina mito mikuu minne, Umba, Sigi, Msangani na Pangani. Mto Pangani upo katika eneo kubwa la Eneo bonde la Pangani eneo la kilomita za mraba 42,200 katika mkoa wa Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

Sheria inayotumika ya kuongoza mifumo ya maji ni ya mwaka 1974 kifungu No. 42. chini ya Kifungu kidogo cha 14 cha sheria hii, mtu yeyote haruhusiwi kutoa tawi, kujenga bwawa, kuhifadhi, au kutumia maji kutoka katika vyanzo vya maji bila kuwa na kibali au kuomba kibali cha maji. Atakayekiuka sheria itamuadhibu.

Kibali cha maji kinatolewa ruhusa kutumia maji kwa kusudio maalumu. Ni hati inayotambulika kisheria inayoruhusu kutoa maji kiasi fulani toka kwenye chanzo cha maji. Watumia maji hulazimika kulipia ada ya kila mwaka kulingana na kiasi cha maji walicholipia. Kipimo cha maji ni mtiririko wa lita za maji kwa sekunde au mita za ujazo kwa sekunde.

Kibali cha kutumia maji hutolewa na ofisi Pangani (Pangani Basin Water Office). Waombaji wa kibali hutambuliwa kisheria pale watakapopata kibali na kulipia ada za kila mwaka kulingana na kiasi cha maji walichogawiwa. Ada ya maombi ya kibali cha kutumia maji ipo katika viwango vitatu tofauti; wakulima wadogo, wakulima wakubwa na wakulima wafanyabiashara (wakulima wakubwa wa maua wanaouza nje ya nchi.

Maombi

Ada	Matumizi
40,000/=	Nyumbani, mifugo, umwagilia mdogo na ufugaji wa samaki.
150,000/=	Umwagilaji mkubwa, uzalishaji wa umeme, viwandani, uchimbaji wa madini, usafirishaji.

Utaratibu wa maombi ya kibali cha maji

Kabla ya kibali kutoka, taratibu zifuatazo ni lazima kufuatwa

1. Jaza fomu ya kuomba kibali na kuituma Ofisi ya Maji ukiambatanisha na ada ya maombi
2. Maombi yatachapishwa kwenye gazeti la serikali
3. Afisa wa maji atachukua maoni kutoka kwa yeyote ambaye ataathirika kutolewa kwa kibali.
4. Afisa wa maji ataambatanisha taarifa kutoka kwa afisa wa serikali wa eneo husika pamoja na maoni na kuwasilisha kwa mshauri wa bodi ya maji.
5. Afisa wa maji atatoa kibali cha maji baada ya kupata mapendekezo ya Bodi
6. Afisa wa maji atamweleza mwombaji iwapo maombi yake yamewekewa pingamizi
7. Mwombaji anaweza kukata rufaa kwa Waziri anayehusika na maji kama hatakubaliana na maamuzi ya Bodi ya Maji.

Ada ya kutumia maji

Wamwagiliaji wadogo

35,000/=	Kwa kipimo kisichozidi lita 3.7
35/=	kwa kila mita za ujazo 100 matumizi ya maji yanayozidi au sawa na lita 3.7

Wamwagiliaji wakubwa

35,000/=	Kiwango kisichozidi lita 18.5
70/=	Kwa kila mita za ujazo 1000 matumizi ya maji yanayozidi au sawa na lita 18.5

Sheria imetamka wazi kuwa, kibali cha kutumia maji hakimpi mtumia maji uhakika kupata maji. Kwa mfano, kipindi cha ukame, Afisa wa maji anaweza kumzuia mtumi maji kuendelea kutumia maji kutoka kwenye chanzo. Zuio hili huwasilishwa kwa watumia maji kwa maandishi.

Sheria ya maji ina faida katika umilikaji wa vyanzo vya maji. Kwanza, sheria imeeleza kuwa maji ni rasilimali ya taifa na si mali ya watu wachache. Inatoa nafasi kwa Watanzania wote kuyatumia. Pili, kila toleo kutoka katika mto Pangani limesajiliwa, lipo kwenye ramani na kuhifandiwa katika hifadhi ya takwimu. Taarifa hizi zinaweza kutumika ili kuweza kufanya maamuzi. Tatu, ukiwa na hati ya kutumia maji na kulipia ada ya mwaka kunawafanya watumia maji kuyathamini maji na kuyatumia kwa uangalifu. Mwisho, hati ya kutumia maji inapunguza migogoro. Kwa mfano, umoja wa watumia maji hutengeneza ratiba ya kugawana maji.

Hati ya matumizi ya maji ni mojawapo ya njia zitakazotuhakikishia kupatikana kwa maji kwa sasa na kwa vizazi vijavyo. Aidha, uvunaji wa maji ya mvua, urejeshaji wa majitaka na uondoshaji wa chumvi katika maji ya bahari kutasaidia upatikanaji wa maji zaidi.